**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA KIDATO CHA TATU**

**KISWAHILI**

MsomiBora.com

**Muda: Saa 03** **i/Juni, 2026**

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu A,B na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili kutoka sehemu C.
3. Sehemu Aina alama (16),sehemu Balama(54)na sehemu C inaalama(30).
4. Zingatia maelezo ya kila sehemu na yakila swali.

**SEHEMU A (16 marks)**

1.Chagua herufi ya jibu sahihi kisha uandike kwenye karatasi ya kujibia

i. Neno linalo ingizwa katika kamusi kwa wino uliokolezwa, fasihi matamshi na aina ya neno hilo kwa pamoja huitwaje?

A. Kidahizo B. Kategolia C. Fasihi D. Istilah

ii.Tamathari za semi inayotumika kufananisha vitu bila kiunganishi inaitwa.

A. Tashihisi B.Tashititi C. taniaba D. sitiari

iii.Mashaili yenye mishororo miwili katika ubeti huitwa.

A. Tarbia B. tathlitha C. tathnia D. Tathmina.

iv.Hamsini,laki, kasri,na filan ni miongoni mwa maneno yanayo thibitisha asili ya Kiswahili ni.

A.Pijini B. Kibantu C. Kiarabu D. Chotara.

v.Kimapokeo, nomino inayojitokeza upande wa kiarifu inaitwa.

A. Chagizo B. Kiarifu C. Prediketa D. shamrisho

vi.Mende anapenda kula uchafu. Neno lililo pigiwa mstari lipo katika ngeli ipi?

A. KI-VI B. U-I C. YU-A-WA D.KU

vii.Ni jambo gani linalo dhihirisha upekee wa kazi fulani ya kifasihi?

A. Jina la mtunzi
B. wahusika
C. . Mtindo
D. .muundo.

viii. Upachikaji wa viambishi katika mzizi wa maneno huitwa.

A. Utohoaji B. Viambishi C. Mnyambuliko D. Uambishaji.

ix.Tofauti ndogo ndogo zinazo jitokeza katika lunga moja huitwa:

A. Kiimbo B. kibantu C. lahaja D. Lunga za kikanda.

x.“Huzuka na kutoweka”ni sifa moja wapo ya

A. Vitendawili B. Misimu C. Rejesta D. sanaa.

2. Oanisha orodha A na orodha B

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i.Kiswahili kilianza kaskazini mashariki mwa Kenya. | A. 1985 |
| ii.Kiswahili kilianza pwani ya Afrika mashariki | B. 1971 |
| iii.Kiswahili kilianza lamu | C. 1 na ya 2 |
| iv.Kiswahili kilianza katika visiwa vya ngozi. | D. 2002 |
| v.Kiswahili kilianza shungwaya kuu. | E. 1994 |
| vi.wabantu waliingia nyanda za kati za kati za Afrika ya | F. 1807 |
| mashariki karne ya | G. 1993 |

| i | ii | iii | iv | v | vi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**SEHEMU B (54 mark)**

3. (a) Maana ya ngeli za nomino

(b).Tunga sentensi mbili kwa kila ngeli zifuatazo.

i.U-I

ii.LI-YA

iii.I-ZI

iv.YU/A-WA

4. (a).Taja hatua tano za uchanganuzi wa sentesi.

(b).changanua sentesi ifuatayo kwa njia ya ngoe kwa kutumia mkabala wa kimapokeo ‘’kenge aliyekatwa mkia ameingia shimoni’’.

5.(a).Utata katika mawasiliano huweza kusababishwa na mambo mengi. Taja mambo matatu yanayosababisha utata katika mawasiliano.

(b).Utata katika tungo za Kiswahili unaweza inaweza kuondolewa kwa namna gani?Taja njia tatu.

6.(a) Kwa ufupi eleza maana ya kirai.

(b) Jambo pekee linalotofautisha aina moja ya kirai na aina nyingine ni muundo wa wake kwa kuwa naneno kuu yenye uhusiano na vijalizo vyake.Kwakutumia mifano eleza miundo mine ya kirai nomino

7.Bainisha shina katika maneno yafuatayo kwa kupigia mstari

(a) Tulikula

(b) Anacheza

(c) Anaimba

(d) atalima

(e) Wanapigana

**SEHEMU C ( 30 mark)**

**Jibu maswali mawili tu katika hii sehemu swali la nane (8) ni lazima**

8.“Kiswahili ni kibantu kwa asili yake fafanua kauli hii kwa kutumia hoja nne za kiisimu

9.Waandishi wengi huandika kazi zao kwa lengo la kutoa ujumbe katika jamii Kwa kutumia tamthiliya mbili moja uliyosoma.Thibitisha ukweli wa kauli hii

10.Mwandishi wa kazi za fasihi hatungi kazi yake kutoka katika ombwe bali kwa kuangalia mambo halisi yaliyo katika jamii yake Thibitisha kauli hii kwa kutumia riwaya moja kati ya riwaya ulizosoma